**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA RUKWA**
**Anuani ya Simu: "REGCOM"**
*Simu Na:025-/2802138/2802144*
**Nukushi (025) 2802217**
Barua pepe: ras@rukwa.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
1 Barabara ya Mkoani,
S.L.P. 128,
**Sumbawanga,**
**55180 RUKWA.**

26 Septemba, 2025

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA KUHUSU MAPOKEZI NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MKOANI RUKWA MWAKA 2025

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa tukiwa na afya njema. Pia, napenda kuwashukuru kwa kuitikia mwaliko huu wa kushirikiana nasi katika kuhabarisha umma kuhusu maandalizi ya mapokezi na mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2025 katika Mkoa wetu wa Rukwa.

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Mkoa wa Rukwa unatarajia kupokea Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa Mwaka 2025 siku ya **Jumapili, tarehe 28 Septemba 2025**, katika **Kijiji cha Kizi, Kata ya Paramawe, Tarafa ya Namanyere, Wilaya ya Nkasi**.

**Ndugu Wanahabari,** Mwenge wa Uhuru ukiwa Mkoani Rukwa utakimbizwa kwa muda wa **siku nne** katika Halmashauri zote nne za Mkoa wetu wa Rukwa ambapo **Tarehe 28 Septemba, 2025** utakimbizwa (Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi), **Tarehe 29 Septemba 2025** (Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga), **Tarehe 30 Septemba 2025** (Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo) na **Tarehe 01 Oktoba 2025** (Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga).

**Ndugu Wanahabari,** Baada ya Mwenge wa Uhuru ukimaliza Mbio zake Mkoani Rukwa, utakabidhiwa rasmi kwa ndugu zetu wa Mkoa wa Songwe tarehe **02 Oktoba 2025** katika **Kijiji cha Kamsamba**.

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Mwenge wa Uhuru ukiwa Mkoani Rukwa utakimbizwa umbali wa **Kilomita 653.1** ambapo utakagua, kuweka mawe ya msingi, na kuzindua **Miradi 34** yenye thamani ya shilingi **Bilioni 55.3.** Kati ya Miradi hiyo **07 itazinduliwa, Miradi 15 itawekwa mawe ya Msingi na Miradi 12 itakaguliwa.**

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Mwenge wa Uhuru mwaka huu una ujumbe maalumu unaohusu **Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025**, chini ya kaulimbiu isemayo **"Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu".**

Ujumbe huu unalenga kuwakumbusha wananchi wote waliojiandikisha na wanaostahili kupiga kura kutumia haki yao ya kikatiba kwa kujitokeza kwa wingi tarehe **29 Oktoba 2025** kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu.

Mbali na ujumbe huo maalumu, Mwenge wa Uhuru 2025 utaendelea kusisitiza mapambano dhidi ya changamoto mbalimbali za kijamii na kiafya, ikiwemo:

- VVU/UKIMWI: *"Chagua Njia Sahihi, Tokomeza UKIMWI"*
- Malaria: *"Ziro Malaria Inaanza na Mimi – inaanza na wewe, inaanza na sisi sote"*
- Dawa za Kulevya: *"Kataa Dawa za Kulevya; Timiza Malengo Yako"*
- Rushwa: *"Kuzuia Rushwa ni Jukumu langu na lako; Tutimize Wajibu Wetu"*
- Lishe: *"Mtaji Ni Afya Yako, Zingatia Unachokula"*

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kujitokeza kwa wingi katika mapokezi na Mbio za Mwenge wa Uhuru 2025. Ushiriki wa wananchi siyo tu kuenzi historia ya Mwenge wa Uhuru, bali pia ni fursa ya kueneza ujumbe wake, kukuza mshikamano wa Taifa letu na kuchochea maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Wananchi wote tushiriki kwa **amani, mshikamano na**

**ushirikiano** na **utulivu** kuupokea Mwenge wetu wa Uhuru na kuukimbiza katika Halmashauri zetu.

**Ndugu Waandishi wa Habari,** Mwisho lakini si kwa Umuhimu niwashukuru sana ninyi Pamoja na Wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kwa ushirikiano wanaonipatia hasa tunapokuwa na Matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na tunapo wapokea viongozi wa Kitaifa. Naomba ushirikiano huo uendelee ili tuendeleze utamaduni wetu wa Rukwa yetu yenye ushirikiano na Mshikamano.

**Mungu Ibariki Tanzania,**

**Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa.**

**Ahsanteni Sana kwa kunisikiliza.**

**Charles Makongoro Nyerere**

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**